## HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI
## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO CHA KUJADILI TAARIFA ZA MWEZI AGOSTI 2023 CHA TAREHE 08/09/2023

MAHUDHURIO

A: WAJUMBE

| S/N | JINA | CHEO | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe Pancras Maliyatabu | -Diwani Kata ya Mtenga (M / Kiti wa Halmashauri | -Mwenyeki |
| 2. | William Mwakalambile | -Mkurugenzi Mtendaji(W) | -Katibu |
| 3. | Mhe: Stephen Kayogolo | -Diwani kata ya ~~Isunta~~ Isale | -Mjumbe |
| 4. | Mhe: Privatus Yolam | -Diwani Kata ya Kala | -Mjumbe |
| 5. | Mhe: Loswiata Sululu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 6. | Mhe: Emiliana Kauzeni | - Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kate | -Mjumbe |
| 7. | Mhe: Francis Nkoswe | -Diwani Kata ya Ntuchi | -Mjumbe |
| 8. | Mhe: Kudra Ahamad | -Diwani Kata ya Isunta | -Mjumbe |
| 9. | Mhe: Kakuli Seba | -Diwani Kata ya Kirando | -Mjumbe |
| 10. | Mhe: Vitalis Malipesa | -Diwani Kata ya Korongwe | -Mjumbe |
| 11. | Mhe: Mpemba Evarist | -Diwani Kata ya Nkandasi | -Mjumbe |
| 12. | Mhe Gorge Saninga | -Diwani Kata ya Myula | -Mjumbe |
| 13. | Mhe: Aida Khenani | -Mbunge Jimbo la Nkasi kaskazini | -Mjumbe |

WASIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe Vicent Mbogo | -Mbunge Jimbo la Nkasi Kusini | -kwa Taarifa |

B WATAALAM

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg Joseph Chasuka | Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W) |
| 2. | Dr. John shauri Tlatlaa | Afisa Mifugo na Uvuvi(W) |
| 3. | Ndg. Dafrosa Mkenda | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 4. | Ndg. Augustine Bayo | Afisa Elimu Msingi(W) |
| 5. | Ndg. Ladislaus Mzelela | Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika(W) |
| 6. | Ndg. Mayuma Nzilantuzu | Afisa Mazingira na Udhibiti TakaNgumu(W) |
| 7. | Ndg. Lucas Mhigi | KaimuAfisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 8. | Ndg. Vicent Magendela | Afisa Mtendaji Mkuu Mamalaka ya Mji Mdogo Namanye |
| 9. | Ndg. Japheth Chuvaka | Kaimu Afisa Maliasili na Uhifadhi Mazingira (W) |
| 10. | Ndg. Albart Mipata | Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi(W) |
| 11. | CPA Erick Kilimo | Mweka Hazina (W) |
| 12. | Ndg. Juma Mlenga | Mthibiti Mkuu ubora wa Shule (W) |
| 13. | Ndg. William Mbinile | Kaimu Mratibu wa TASAF (W) |
| 14. | Ndg. Atufigwege Mwakitega | Kaimu Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W) |

| | | |
|---|---|---|
| 15. Ndg. Salu | Makoye | Kaimu Mkaguzi Wa Ndani (W) |
| 16. Ndg. Richard | Katyega | Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu |
| 17. Ndg Benjamini | Chota | Mganga Mkuu(W) |
| 18. Ndg. John | Ntulo | Kaimu Afisa TEHAMA (W) |
| 19. Eng Gido | Monji | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |
| 20. Ndg. Didas | Sadan | Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri |

B: SEKRETARIETI

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Rashid | Ahmad | Kaimu Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri |
| 2. Ndg. John | Mnungwasa | Mhudumu wa ofisi |

AGENDA NA NKS/DC/FUM/01/09/2023

KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5.15 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe waliohudhuri na kusisitiza wajumbe kuchangia mawazo kwa kadri ya agenda zilivyoandaliwa n kuwasilishwa mbele yao kwa maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

AGENDA NA NKS/DC/FUM/02/09/2023

KUTHIBITISHA AJENDA

Wajumbe walithibitisha agenda.

AGENDA NA NKS/DC/FUM/03/2023

KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA

Wajumbe waliupitia muhtasari wa kikao kilichopita ukurasa kwa ukurasa na kufanya marekebisho yaliyojitokeza kisha walikubali muhtasari uwekwe saini kama kumbukumbu sahihi ya kikao kilichopita.

AGENDA NA NKS/DC/FUM/04/09/2023

YATOKANAYO NA KIKAO KILICHOPITA

**Kuhusu Halmashauri kutoa fedha kwa ajili ya kutengeneza Nkasi Fm Radio.**

- Mjumbe alitaka kujua kama Nkasi FM imeshaanza kufanya kazi
- Mjumbe alishauri Redio hiyo iongezewe masafa ili na maeneo mengine yaweze kupata matangazo.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alifafanua kuwa Redio hiyo imeshatengenezwa na tayari mawasiliano yameshafanyika na TBC ili kuona namna ya kuongeza masafa ya Redio Nkasi FM.

**Kuhusu kuweka vyanzo vya mapato kwenye mfumo ya kukusanyia mapato (Poss Machine) ambavyo havipo kwenye Poss.**

- Mjumbe alitaka kujua sababu ya vyanzo hivyo kutowasilishwa Ofisi ya Raisi TAMISEM mpaka sasa hali inayopelekea mapato ya Halmashauri kupotea.
- Baada ya hoja hiyo kuibuka Mkurugenzi Mtendaji (W) alifafanua kuwa mawasiliano yameendelea kufanyika ili kuweza kuongeza vyanzo hivyo vya mapato

Baada ya maelezo hayo kikao kiliazimia kama ifuatavyo

**Azimio**

**Utaratibu ufanyike kwa kuwasiliana na Ofisi ya Raisi TAMISEM ili vyanzo ambavyo havijaingizwa kwenye POSS Viingizwe ili kuongeza mapato ya Halmashauri**

AGENDA NA NKS/DC/FUM/05/09/2023

TAARIFA YA MPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI 2023

Kaimu Mweka hazina (W) aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Agosti 2023, na kusisitiza kuwa kwa kpindi cha Mwezi Julai hadi Agosti 2023 Halmashauri imekusanya jumla ya Tsh 441,081,349.

Aidha Halmashauri kwa mwezi Julai mpaka Agosti 2023 ilipokea fedha ya ruzuku kutoka serika kuu jumla ya Tshs 2,238,023,284 sawa na silimia 19 ya makisio ya mwaka na imetumia jumla ya Tshs 221,327,500 sawa na asilimia 21 ya makisio.

Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia hoja kama ifuatavyo;

- Mjumbe alisitiza kuwa ni vyema jitihada zaidi zikafanyika ili kuongeza mapato ya Halmashauri, ikiwa ni pamoja na kuziba mianya ya utoroshaji wa mapato, pia kuhakikisha Boti za Halmashauri zinafanya kazi lengwa badala ya mapato kutoroshwa
- Mjumbe alishauri wakusanya mapato wanatakiwa kuwa waadilifu ili mapato yasiweze kupotea
- Mjumbe aliomba wakusanya mapato wanaotokana na JKT wakawa wanabadilishwa mara kwa mara ili kudhibiti utoroshwaji wa mapato.

Baada ya hoja za wajumbe Mkurugenzi Mtendaji (W) alifafanuwa kuwa watoza ushuru wataendelea kubadilishwa ili kudhibiti ukusanyaji wa mapato, na kusisitiza kuwa ushirikiano unatakiwa uwepo baina ya wataalamu na viongozi wa kisiasa ili kuongeza mapato ya Halmashauri katika ukanda wa Ziwa Tanganyika

Wajumbe walipokea ufafanuzi huo na kuagiza wakusanya mapato wanaofanya vizuri katika ukusanyaji wapewe motisha ili kuongeza mapato ya Halmashauri ,pia walisisitiza mashine za kukusanyia mapato (POSS mashine) zinunuliwe ili kila kituo kinachokusanya kiwe na mashine ya kukusanyia

## AGENDA NA NKS/DC/FUM/06/09/2023
## KUHUSU KUPITIA MATUMIZI YA MWENGE WA UHURU

Kaimu Mweka hazina (W) aliwasilisha taarifa ya matumizi ya mwenge wa uhuru 2023 na kufafanua kuwa jumla ya Tshs 59,872,600/= zilitumika, ambapo Tshs 44,574,800/= zilitumika kama matumizi ya kawaida na Tshs 15,297,800/= kwa ajili ya ununuzi wa mafuta.Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

- Mjumbe alitaka kujua kiasi kilichotengwa kwa ajili ya shughuli za mwenge wa uhuru
- Mjumbe alishauri kuwa wakati mwingine kikao cha dharula kikaitishwa ili kujadili mapato na matumizi ya mwenge ili kamati ijue na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.
- Ushauri kutoka kwa mjumbe mwingine ilikuwa ni kuwa ni vema akaunti ya Mwenge ikafunguliwa ili fedha za mwenge ziwe zinatunzwa katika akaunti,.

Baada ya majadiliano ya kina Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa agenda ya mapato na matumizi ya Mwenge wa uhuru itakua inajadiliwa mwezi juni kwa kila mwaka. Wajumbe walipokea na kuunga mkono hoja

## AGENDA NA NKS/DC/FUM/07/09/2023
## KUHUSU MAPOKEZI YA KIFAA CHA KUPIMA UDONGO (SOIL SCANNER)

Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W) aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya kifaa cha kupimia udongo (soil scanner) na aliwaeleza wajumbe kuwa lengo la kifaa hiki ni kupima

afya ya udongo na kujua mazao yanayotakiwa kulimwa katika eneo husika. Aliendelea kusisitiza kuwa maafisa ugani watapewa maelekezo mahususi ili kujua namna ya kutumia kifaa hicho na utaratibu utawekwa ili kila anae hitaji kupimiwa udongo katika shamba lake aweze kupimiwa. Hivyo kila Afisa Ugani atatakiwa kuleta udongo wa mashamba kutoka kwenye mashamba ya wakulima katika maeneo yao na kusisitiza kuwa upimaji wa udongo utakuwa ni bure. Aidha aliendelea kusisitiza kuwa msimu huu bei za mbolea itakua ni kama ifuatavyo; DAP = 77,800,/= UREA = 67,700/= na CAN 71,000/=

Baada ya maelezo hayo wajumbe walipokea taarifa na walichangia kama ifuatavyo;

- Mjumbe aliomba ikiwezekana nakala za bei za mbolea ya ruzuku zigawiwe kwa Waheshimiwa Madiwani ili waweze kutoa elimu kwa wananchi wake kuhusu bei hizo kulingana na maeneo,.
- Mjumbe alitaka kujua muda utakaotumika kwa kifaa cha kupimia udongo kutoa majibu husika.
- Mjumbe alitaka kujua hatua zinazotakiwa kuchukuliwa dhidi ya mvua za elinino ili kulima kilimo chenye tija.
- Mjumbe alitaka kujua mbinu zitakazotumika ili maeneo ambayo hakuna maafisa ugani waweze kupata huduma ya kupimiwa udongo.

Baada ya hoja mbalimbali kuibuliwa Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika(W) alifafanua Hoja za wajumbe kuwa Mafisa ugani ndio watakaotumika katika kupima udongo au kwa kutumia maafisa ugani walioko Ofisi ya Wilaya, pia wanaotaka pembejeo za kilimo kama trekta watatakiwa kuomba kwenye kampuni husika kupitia Ofisi ya kilimo ya (W), Aidha kuhusu bei ya mbolea kutolewa kutokana na umbali eneo liliko ambapo mjini bei itakua ndogo na kata ya kala bei itakua kubwa zaidi, na kipimo cha udongo hutoa majibu hapohapo. Baada ya ufafanuzi huo wajumbe waliunga mkono hoja

**AGENDA NA NKS/DC/ FUM/08/09/2023**

**TAARIFA YA HESABU ZAMWISHO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 08/09/2023.**

Kaimu Mwekahazina (W) aliwasilisha taarifa ya hesabu za mwisho za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 08/09/2023,

Kisha wajumbe kwa kauli moja waliunga mkono hoja.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/09/09/2023**

**MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

1. Kuhusu suala la kamati ya fedha kupewa semina kuhusu namna ya kutekeleza majukumu ya kamati.

- Mjumbe alisisitiza kuwa ni vyema kamati ya Fedha Utawala na Mipngo ikapewa semina ili kila mwanakamati aelewe majukumu yake.

Baada ya maelezo hayo wajumbe waliagiza kma ifuatavyo;

Agizo;

Mkurugenzi Mtendaji (W) aone namna ya kutoa semina kwa wajumbe wa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ili kila mjumbe ajue wajibu wake

**AGENDA NA NKS/DC/CMT/10/09/2023**
**KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 11.07 jioni.

MUHTASARI
UMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA

……………………………..
WILIAMU MWAKALMBILE
KATIBU

……………………………..
PANCRAS MALIYATABU
MWENYEKITI

TAREHE 10/11/2023